NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

29 Desemba 2015

Kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara

Marafiki wapendwa sana,

1. Mpango ambao ulimwengu wa Kibaha'i uliuanza takribani miaka mitano iliyopita upo katika hatua za umalizikaji wake; hesabu ya mwisho ya mafanikio yake bado inakua, lakini hivi punde itafungwa. Juhudi ya pamoja ulioihamasisha imehitaji kutegemea kwa moyo mkunjufu kwenye nguvu ambazo kwazo Bwana mkarimu amewajalia wapendwa Wake. Tukikusanyika pamoja nanyi katika wakati huu wa tafakari, tunatambua azma miongoni mwa marafiki kuuleta Mpango wa hivi sasa kwenye hitimisho linalostahili, na ya shauku kuiendeleza mbele zaidi njia ambayo uzoefu umeionesha.

2. Umbali mkubwa ambao tayari umepitwa katika njia hiyo uko dhahiri kutokana na matokeo ya kuvutia kabisa ya Mpango wa hivi sasa. Lile lengo kuu la uinuaji idadi ya klasta kufikia 5,000 ambamo mpango wa ukuaji, kwenye kiwango chochote kile cha nguvu, linaendelea kuonekana kufanikiwa katika miezi iliyobaki kabla ya Ridvan 2016. Katika korija nyingi za klasta, kuna zaidi ya elfu ya wakazi – mara nyingine maelfu kadhaa - wanaoshiriki katika mtindo wa shughuli uliositawishwa vyema ambao daima hujumuisha idadi kubwa zaidi, ukiinua jumuiya ambazo mazoea yao ya fikra na utendaji vimewekwa imara katika ufunuo wa Baha'u'llah. Ulimwenguni kote, nusu ya milioni ya watu hivi sasa wamewezeshwa kumaliza angalau kitabu cha kwanza katika mfululizo wa kozi, tendo kubwa la ajabu ambalo limeweka msingi wa uhakika kwa ajili ya ukuzaji wa rasilimali watu. Kizazi cha vijana kinaamshwa kutenda kwa muono uvutiao sana wa jinsi wawezavyo kuchangia kwenye ujenzi wa ulimwengu mpya. Wakishangazwa na kile ambacho wamekiona, viongozi wa jamii katika mahali kadhaa wanawashinikiza Wabaha'i kuzifanya program zao kwa ajili ya uelimishaji vijana zipatikane kwa wote. Zikikabiliwa na utata unaoongezeka, asasi za Kibaha'i na mawakala wao zinagundua njia za kuandaa shughuli za idadi zinazokua za marafiki kwa kupitia ushirikiano na usaidizi wa pamoja. Na uwezo wa ujifunzaji, ambao uliwakilisha urithi wa thamani kama huo wa Mipango iliyopita unapanuliwa zaidi ya uwanja wa upanuzi na uimarishaji ukijumuisha maeneo mengine ya jitihada za Kibaha'i, hasa shuhuli za jamii na ushiriki katika mazungumzo yaliyoenea ya jamii. Tunaona jamii iliyoimarishwa kwa vipaji vya nguvu na uzoefu uliopatikana kwa shida ambao hutokana na miongo miwili ya juhudi ya mfululizo iliyolengwa kwenye shabaha ya pamoja: maendeleo ya maana katika mchakato wa uingiaji kwa makundi.

3. Kwamba mchakato huu lazima uende mbali zaidi, hapawezi kuwa na shaka; hata hivyo, maendeleo yanaonesha kwamba upigaji hatua muhimu tayari umekwishatokea. Umewaandaa

marafiki wa Mungu kwa ajili ya jaribio shurutishi zaidi la uwezo wao, lile ambalo pia litahitaji sana asasi yenu kadiri muwakusanyavyo kutimiiza mahitaji yake. Katika Mpango huu ujao, ambao utamalizika kwenye kilele cha karne ya pili ya zama za Ujenzi wa Imani, tutawaita waumini kila mahali kwenye jitihada kubwa mno ihitajikayo kuzilete kwenye utoaji matunda mbegu ambazo zimepandwa kwa upendo mwingi mno na uangalifu na kumwagiliwa maji katika Mipango mitano iliyoutangulia.

***Uibukaji wa mpango wa ukuaji***

4. Ukunjukaji wa mchakato wa ukuaji katika klasta, wakati kiasili ukiwa na sura za kipekee katika kila namna ifanyizwayo na upokevu wa wale ambao wametambulishwa kwenye mafundisho matakatifu, hukubaliana na tabia kadhaa zinazoendana. Nyingi ya hizi zilijadiliwa katika ujumbe wetu kwa kongamano lenu la 2010, ambamo marejeo yaliyofanywa kwenye mfululizo wa hatua ambazo huainisha ukuaji katika njia ya maendeleo. Uelewa wa pamoja wa kile kihitajiwacho kwa marafiki katika kupita hatua ya kwanza tuliyoielezea, na halafu ya pili umekua katika kipindi hiki.

5. Katika Mpango wa Miaka Mitano unaomalizika hivi sasa, kazi inayowakabili waumini imekuwa ni kutumia yale yote waliyojifunza kutoka Mipango iliyopita kwenye kazi ya upanuaji wa mchakato wa ukuaji kwa maelfu ya klasta mpya. Kile ambacho hili limeonesha ni kwamba mengi hutegemea juu ya uwezo wa asasi kuchota kutoka kwenye msaada wa marafiki katika klasta nyingine, kuimarisha vitendo vya jamii ya Wabaha'i iliyopo kwa mfano, kuandaa msaada wa timu za ufundishaji zinazotembelea au wakufunzi. Katika sehemu zingine, mchakato wa taasisi huanza kwa msaada wa waumini kutoka jamii jirani zenye nguvu zaidi ambazo hugundua njia za ubunifu za kufikia idadi ya watu wa mahali, hususan vijana, na kuwasaidia kadiri waanzavyo kujishughulisha katika huduma. Juhudi za kuamsha shughuli katika klasta, hasa ile ambayo haijafunguliwa kwa Imani, zinazidishwa kabisa kama mtu mmoja au zaidi hufanya makazi hapo kama watangulizi wa nyumbani, kumakinikia uangalifu kwenye sehemu ya kijiji au hata mtaa mmoja ambao kuna upokevu mkubwa. Bara bara zaidi ya waumini 4,500 tayari wameinuka kuhudumia katika njia hii wakati wa mpango wa hivi sasa, mafanikio ya kushangaza.

6. Mchanganyiko wowote ule wa mikakati itumiwayo, shabaha kubwa ni kuanzisha mchakato kwa ajili ya ujengaji uwezo ndani ya klasta ambao kupitia huo wakazi wake, wakishawishiwa na shauku ya kuchangia kwenye ustawi wa kiroho na wa kimwili wa jumuiya zao, wanawezeshwa kuanza kufanya vitendo vya huduma. Mara tu hitaji hili la kimsingi likifikiwa, mpango wa ukuaji umekwishaibuka. Jambo la muhimu, bila shaka, ni msaada wa Washauri Wasaidizi na wasaidizi wao, ambao ujihusishaji wao wa karibu kutoka uamshaji wa kwanza wa shughuli huwasaidia marafiki kudumisha muono ulio dhahiri na wa pamoja wa kile kinachohitajika.

*Uimarishaji wa mtindo wa utendaji*

7. Muda si mrefu, huanzishwa kiini cha marafiki katika klasta ambao wanaofanya kazi na kushauriana pamoja na kupanga shughuli. Ili mchakato wa ukuaji uendelee mbele zaidi, idadi ya watu wanaogawana wajibu huu sharti iongezeke, na uwezo wao kwa ajili ya kujitolea kushughulikia utendaji wa kiutaratibu ndani ya mfumo wa Mpango sharti pia uongezeke kiuwiano. Na ukifananishwa na ukuaji wa kiumbe hai, ukuaji waweza kutokea kwa haraka wakati vigezo sahihi vimewekwa.

8. Cha muhimu kabisa miongoni mwa vigezo hivi ni mchakato wa taasisi unaojipatia nguvu, ukipewa umuhimu wake kwenye ukuzaji wa mjongeo wa idadi ya watu. Marafiki ambao wameanza kujifunza nyenzo za taasisi na pia wanaziwekeza nguvu zao katika uandaaji wa madarasa ya watoto, vikundi vya vijana chipukizi, mikusanyiko kwa ajili ya ibada ya pamoja, au shughuli nyingine zihusianazo, wanasaidiwa kuendelea mbele zaidi kupitia mfululizo wa kozi, huku idadi ya wale wanaoanza masomo yao huendelea kuongezeka. Pamoja na mtiririko wa washiriki kupitia kozi za taasisi na kwenye uwanja wa utendaji unaodumishwa, kundi la wafanyao kazi pamoja wanaoudumisha mchakato wa ukuaji hupanuka. Maendeleo hutegemea kwa kiasi kikubwa juu ya ubora wa juhudi za wale wanaohudumia kama wakufunzi. Katika hatua hii ya mwanzoni, wengi wao bado wanaweza kuwa wanachotwa kutoka klasta zingine, lakini wakati huo huo, marafiki wachache wenyeji wanakuwa wanakuzwa ambao, kadiri uwezo wao kwa utendaji uongezekavyo, huanza kuwasaidia wengine kujifunza nyenzo za taasisi. Juhudi za kuanzisha kada ya kwanza ya wakufunzi kutoka katika klasta sharti zielekeze njia baina ya matokeo mawili yasiyofaa. Kama watu wakiendelea kupitia masomo ya taasisi kwa haraka mno, uwezo wa kuhudumia huwa haukuzwi vya kutosha; kinyume chake, kama usomaji ukirefushwa mno, mchakato hunyang'anywa nguvu iliyo muhimu kwa maendeleo yake. Katika hali tofauti, ufumbuzi wa kiubunifu umetumiwa kupata usawa uhitajikao, kuhakikisha kwamba ndani ya kipindi kinachofaa, baadhi ya miongoni mwa wale waishio katika klasta wanawezeshwa kuhudumia kama wakufunzi.

9. Bila shaka, sio utoaji wa mafunzo pekee ambao huleta maendeleo. Juhudi za kujenga uwezo hupungukiwa kama matayarisho hayafanywi kwa haraka kuambatana na watu binafsi kwenye uwanja wa huduma. Kiwango cha kutosha cha msaada huenda mbele zaidi ya maneno ya kutia moyo. Wakati wa kujiandaa kufanya kazi ngeni, kufanya kazi sambamba na mtu mwenye uzoefu fulani huongeza ufahamu wa kile kiwezekanacho. Uhakika wa msaada wa kivitendo unaweza kumpa mtu ajaribuye ujasiri wa kuanzisha shughuli kwa mara ya kwanza. Ndipo roho huendeleza uelewa wao pamoja, kwa unyenyekevu zikishirikiana umaizi ambao kila mmoja anao katika wakati huu na kwa shauku wakitafuta kujifunza kutoka wasafiri wenzao kwenye njia ya huduma. Usitasitaji hurudi nyuma na uwezo hukua hadi pale ambapo mtu anaweza kutekeleza shughuli kwa kujitegemea mwenyewe na, kwa zamu kuambatana na wengine kwenye njia hiyo hiyo.

10. Pale ambapo taasisi inahusika, mtiririko wa washiriki kupitia mafunzo yake hufanyiza haja inayoongezeka kwa wao kusaidiwa kiutaratibu kadiri waanzavyo kuhudumia kama walimu wa watoto, kama wahuishaji, na kama wakufunzi. Fursa huibuka kiasilia kwa wale miongoni mwa kiini cha waumini ambao tayari wamekwisha jipatia kiasi cha uzoefu katika shughuli za kielimu kuwasaidia wale ambao ni wapya zaidi kwao. Utayari wa mtu kuwasaidia wengine kusonga mbele katika juhudi zao kuhudumia unaweza kuongoza kwenye kupewa kwake majukumu mahususi. Kwa jinsi hii, waratibu wa kila mojawapo ya zile hatua tatu za mchakato wa kielimu pole pole huibuka kadiri ya mahitaji yanavyodai. Vitendo vyao wakati wote husukumwa na ile haja ya kuona uwezo ukikua ndani mwa wengine na kulea urafiki juu ya msingi wa ushirikiano na kutendeana.

11. Kwa udhahiri, mchakato wa taasisi hukuza uwezo kwa wigo mpana wa shughuli, kutoka kozi za mwanzoni kabisa, washiriki hutiwa moyo kuwatembelea marafiki zao majumbani kwao na kujifunza sala pamoja au kushirikiana nao wazo kutoka mafundisho ya Kibaha'i. Mipangilio kwa ajili ya kuwasaidia marafiki katika jitihada hizi, ambayo ingeweza kuwa kwa kiasi kikubwa siyo rasmi, hatimaye huthibitisha kuwa isiyokidhi, ikiashiria hitaji kwa ajili ya Kamati ya Ufundishaji ya Eneo kutokea. Lengo lake kuu ni uhamasishaji wa watu mmoja mmoja, mara nyingi kupitia uundaji wa timu, kwa ajili ya uenezaji endelevu wa mtindo wa shughuli katika klasta. Wajumbe wake huja kumuona kila mmoja kama mshirika muhimu katika shughuli ya pamoja, na wao hutambua vyema sehemu yao wenyewe katika uleaji moyo wa lengo la pamoja katika jumuiya. Kwa kuwepo kamati, juhudi ambazo tayari zinaendelea kuitisha mikusanyiko kwa ajili ya ibada, kutekeleza ziara za majummbani, na kufundisha Imani sasa huweza kupanuka kwa kiasi kikubwa. Mtahitaji kuyatia moyo Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na Halmashauri za Kanda za Kibaha'i, vile vile taasisi za mafunzo, kubaki macho juu ya ni wakati gani hali katika klasta hulazimu mipangilio ya kiutaratibu kujitwalia umbo rasmi – wala sio kutenda kabla ya wakati wake wala kuchelewesha bila sababu utokeaji wa miundo rasmi.

12. Kama vile ilivyo kwa watu binfsi, mawakala waibukao katika klasta huhitaji msaada kadiri wajitwaliavyo majukumu yao. Msaada ambao Washauri Wasidizi huutoa kuhusu jambo hili ni muhimu, lakini pia ni jukumu muhimu la Halmashauri za Kanda za Kibaha'i au, pale ambapo Halmashauri haipo, Baraza la Kiroho la Kitaifa lenyewe, na jambo muhimu kwa taasisi za mafunzo hali kadhalika. Uwezo wa kuhudumia kwa ustadi katika ngazi ya klasta huongezeka wakati nafasi hufanyizwa ambamo waumini wanaojihusisha huweza kujifunza mwongozo, hutafakari juu ya vitendo vyao katika mwanga wake na kuchota umaizi kutoka humo, na pia kuunganishwa na mkusanyo mpana zaidi wa ujifunzaji unaozalishwa katika klasta zinazozunguka na mbali zaidi. Badala ya kuunda mipango kinadharia, ushauriano uendeshwao katika nafasi hizo mara nyingi hulenga kwenye kuupata uhalisia wa klasta katika wakati huo mahususi na kuzitambua hatua za mara moja zifuatazo kurahisisha maendeleo. Wale wanaohudumu kwenye ngazi ya Kanda au ya Kitaifa wangeweza kufanya mengi kuwashauri marafiki na kupanua muono wao wa kile kiwezacho kutimizwa, lakini wasingetafuta kulazimisha

matarajio yao wenyewe juu ya mchakato wa upangaji mipango; afadhali, wawe wanawasaidia waumini ambao wanajitahidi katika klasta pole pole kuongeza uwezo wao wa kubuni na kutekeleza hatua za utekelezaji zinazotokana na uzoefu unaojilimbikiza kwenye ngazi ya umma ya jumuiya na kuizoea hali halisi. Ili kukuza uwezo wa mawakala wa klasta kujifunza na kutenda kwa utaratibu, asasi za kanda na za kitaifa huhitaji kuwa makini na zenye utaratibu katika juhudi zao zenyewe kuwasaidia mawakala hao. Msaada wa wasidizi wenu kwa kazi hii utahakikisha kwamba kila sehemu ya mchakato wa ukuaji imefikia sifa bainifu itakiwayo na kwamba ukamilifu na upatano wa juhudi zote hudumishwa.

13. Msukumo wa kujifunza kupitia utendaji umo, bila shaka, miongoni mwa marafiki kutoka mwanzoni kabisa. Utambulisho wa duru za kila robo mwaka za shughuli hutumia uwezo huu uibukao na huuruhusu uimarishwe kwa uthabiti. Ingawa huu uwezo huhusishwa kwa uhalisi na ile awamu ya tafakari na ufanyaji mipango ya duru, hasa mkusanyiko wa tafakari ambao hudhibiti kupuma kwa pigo la moyo wake, huja pia kutumiwa mahali popote pengine pa duru na wale ambao hufuatilia njia zihusianazo za utendaji. Tunatambua kwamba, kadiri ujifunzaji uzidishavyo mwendo, marafiki huwa wenye uwezo zaidi kushinda vipingamizi, viwe vidogo au vikubwa – kubaini kiini cha sababu zake, kuchunguza kanuni za kimsingi, kutumia uzoefu husika, kutambua hatua za kuponya, na kutathmini maendeleo, mpaka mchakato wa ukuaji umetiwa tena nguvu kikamilifu.

14. Jambo kuu kwa muundo wa utendaji unaokua katika klasta ni mbadiliko wa mtu binafsi na wa pamoja usababishwao kupitia nguvu ya Neno la Mungu. Kutoka mwanzoni mwa mfululizo wa kozi, mshiriki hukutana na Ufunuo wa Baha'u'llah katika kufikiria mawzo mazito kama vile ibada, huduma kwa binadamu, maisha ya roho, na elimu ya watoto na vijana. Kadiri mtu akuzavyo tabia ya kujifunza na tafakari ya undani sana juu ya Neno la Uumbaji, mchakato huu wa mbadiliko hujidhihirisha wenyewe katika uwezo wa kuelezea uelewa wake wa dhana za ndani sana na kuchunguza uhalisia wa kiroho katika mazungumzo ya maana. Uwezo huu huonekana sio tu katika majadiliano ya hali ya juu ambayo huzidi kuainisha muingiliano ndani ya jumuiya, lakini katika mazungumzo yaendeleayo ambayo hufika mbali zaidi – si kidogo kati ya vijana wa Kibaha'i na wale wa rika lao – huendelea kujumuisha wazazi ambao binti na vijana wao wanafaidika kutokana na programu za kielimu za jumuiya. Kupitia mabadilishano ya aina hii, ufahamu wa nguvu za kiroho hukuzwa, uwili uonekanao hujiachia kwa umaizi usio tarajiwa, hisia ya umoja na wito wa pamoja huimarishwa, imani kwamba ulimwengu bora unaweza kuundwa huimarishwa, na kujifunga kwa utendaji hudhihirika. Mazungumzo haya ya kipekee pole pole huvutia daima idadi kubwa zaidi kushiriki katika mlolongo wa shughuli za jumuiya. Dhamira za imani na yakini kiasili huibuka, zikishawishiwa na upokevu na uzoefu wa wale wahusikao. Kilicho dhahiri, basi,ni kwamba kadiri ya mchakato wa taasisi katika klasta upatavyo mwendo, kitendo cha ufundishaji huja kujitwalia umashuhuri zaidi katika maisha ya marafiki.

15. Kadiri maendeleo yasongavyo mbele, uwezo unaoinuka kwa ajili ya mazungumzo ya maana hutumiwa katika mipango ya asasi. Wakati duru za shughuli zimeibuka rasmi, uwezo huu

huchochewa zaidi kupitia kipindi cha upanuzi ambayo kwa kiasi kikubwa huamua matokeo ya kila duru. Shabaha hasa za kila kipindi cha upanuzi hutofautiana, bila shaka, kutegemea juu ya hali katika klasta na hali za jumuiya ya Kibaha'i. Katika namna fulani, shabaha yake ni kuongeza ushiriki katika shughuli za kimsingi, katika nyingine, utayari wa kujiandikisha katika Imani hugunduliwa. Mazungumzo juu ya Utu wa Baha'u'llah na azma ya ujumbe Wake hutokea katika mazingira mbalimbali, yakijumuisha fayasaidi na ziara za majumbani. Shughuli zifanywazo katika kipindi hiki huruhusu uwezo uliokuzwa kutokea kujifunza dhana husika za taasisi kufanyiwa mazoezi na kuboreshwa. Kadiri uzoefu ukuavyo, marafiki huwa stadi zaidi katika kutambua wakati gani wamelipata sikio sikivu, katika kuamua ni wakati gani wa kutumia njia ya moja kwa moja zaidi katika kushirikiana ujumbe, katika kuondoa vikwazo kwa uelewa, na katika kuwasaidia watafutaji kuikubali Hoja. Njia ya ufanyaji kazi katika timu huwaruhusu marafiki kuhudumu pamoja, kutoa usaidizi wa pamoja, na kujenga kujiamini – lakini hata wakati wa utekelezaji wa shughuli kwa mtu mmoja mmoja, wanaratibu juhudi zao kwa matokeo makubwa zaidi. Fokasi yao na uwekezaji wao wa muda huijalia awamu hii fupi lakini cha mkataa cha duru nguvu kinayoihitaji. Moyo huu wa azma ya hali ya juu husaidia kuzidisha nguvu za jamii, na katika kila duru marafiki hujifunza kutegemea zaidi na zaidi juu ya mathibitisho ya nguvu kutoka milki takatifu ambayo vitendo vyao huvutia.

16. Miaka mitano iliyopita, klasta nyingi kabisa ambamo mpango wa ukuaji wenye nguvu ulikuwa umeanzishwa zilikuwa zile ambamo idadi ya kutosha ya Wabaha'i tayari waliishi, mara nyingi wakitawanyika kijiografia. Juhudi kwa upande wa waumini hao kuendeleza mbele kazi kwa kukaribisha ushiriki wa marafiki, wafanyakazi wenzi, ndugu wa kifamilia, na jamaa zilifanya mengi kuinua kiwango cha shughuli kwenye klasta nzima. Naam, upanuzi wa duru la ushiriki katika njia hii kimekuwa kipengele kifahamikacho cha maisha ya Kibaha'i na hubakia muhimu. Wakati huo huo, uzoefu huonesha kwamba, ili ukuaji uchapuzwe kupitia mtiririko madhubuti wa washiriki wapya wanaoingia katika mchakato wa taasisi, mengi zaidi huhitajika. Mtindo wa maisha ya jumuiya sharti uendelezwe katika mahali ambapo upokevu hufurika, vile vituo vidogo vya idadi ya watu ambamo shughuli ya nguvu inaweza kudumishwa. Ni hapa, wakati kazi ya ujengaji jumuiya hutekelezwa ndani ya mzingo finyu, kwamba vipimo vinavyoingiliana vya maisha ya jumuiya hushughulikiwa kwa upatano zaidi, kwamba mchakato wa mbadiliko wa pamoja huhisiwa kwa shauku kali sana – hapa kwamba, ndani ya muda, nguvu ya ujengaji jamii iliyo asili katika Imani hudhihirika kabisa.

17. Kwa hiyo, kazi muhimu inayowakabili ninyi na wasaidizi wenu mwanzoni kabisa mwa Mpango hujao itakuwa ni kuwasaidia marafiki kila mahali kutambua vyema kwamba- ili mipango iliopo ya ukuaji iendelee kupata nguvu, mkakati wa uanzishwaji wa shughuli za ujengaji jumuiya katika ujirani na vijiji ambavyo huonesha matumaini lazima uchukuliwe kwa mapana na ufuatiliwe kiutaratibu. Watu binafsi wanaohudumu katika maeneo kama hayo hujifunza jinsi ya kuelezea makusudi ya shughuli hizo, kuonesha kwa matendo usafi wa nia zao, jinsi ya kulea mazingira ambapo wale wasitasitao wanaweza kuhakikishiwa tena, jinsi ya

kuwasaidia wakazi kuuona uwezekano mwingi ufanyizwao kwa ufanyaji kazi pamoja, na jinsi ya kuwatia moyo kuinuka kuhudumia maslahi bora kabisa ya jamii yao. Bado, utambuzi wa thamani halisi wa kazi hii lazima pia uongeze ufahamu wa uwelekano wa kusababisha madhara. Mtindo wa utendaji uibukao katika eneo dogo unaweza kuzimwa kwa urahisi kwa uangalifu uliokithiri kutoka nje; kulingana na hili, idadi ya marafiki ambao huhamia sehemu kama hizo au huwatembelea huko mara kwa mara haihitaji kuwa kubwa kwa sababu, hata hivyo mchakato unaoanzishwa kimsingi ni ule utegemeao wenyeji wenyewe. Kinachohitajika kutoka kwa wale wanaojihusisha, walakini, ni kujitoa kwa muda mrefu na shauku kujizoeza mno na uhalisia wa sehemu ambamo wao hujifungamanisha na maisha ya eneo na wakiepukana na dalili yoyote ya chuki au ubaba, hufanyiza vile vifungo vya urafiki wa kweli ambavyo huwastahili waliowenzi katika safari ya kiroho. Nguvu ambayo hukua katika mazingira kama hayo hufanyiza hisia yenye nguvu ya nia ya pamoja na usongaji mbele. Baada ya muda, klasta nzima na vituo vyake vya shughuli ya nguvu vitajaziana ufahamu ulioinuliwa ambao huja kutokana na juhudi kutumia mafundisho katika muktadha tofauti tofauti.

18. Kadiri marafiki katika klasta waendeleavyo kuimarisha na kupanua shughuli za ujengaji jumuiya zipatazo umbo zinazowazunguka, huja kudhihirika kwamba upigaji hatua wa kipekee umefanyika. Vipengele vyote muhimu vya mfumo kwa ajili ya kudumisha ukuaji sasa vipo mahali pake. Ufikiaji wa hatua ya pili ya ukuaji katika mwendelezo wa maendeleo, ambao tuliwaelezea miaka mitano iliyopita, husindikizwa na kukua kiidadi na pia kiubora - kama vile ongezeko katika idadi ya wale wanaojihusisha katika mazungumzo ambayo huwezesha upokevu kugunduliwa na kulelewa, katika nyumba ngapi zinaendelea kutembelewa, katika shughuli za msingi na ushiriki, katika idadi gani ya watu wanaoanza mfululizo wa kozi au wanaowasaidia wengine kadiri wapatavyo ujasiri kuhudumia. Mahudhurio kwenye mikusanyiko kuashiria Karamu ya Siku Kumi na Tisa na Siku Takatifu za Kibaha'i hukuzwa na Mabaraza ya Kiroho ya Mahali. Hatua kama hizo ni ishara zionekanazo zaidi za maendeleo mengi bora zaidi; ueneaji wa pole pole, ndani mwa idadi ya watu, wa muundo wa maisha ya jumuiya yaliyotegemezwa kwenye mafundisho ya Baha'u'llah. Na, kiasili, idadi ya waumini hukua.

19. Katika miaka mitano iliyopita, njia iongozayo kwenye uibukaji wa mpango wa ukuaji wenye nguvu imekuwa ikionekana zaidi kwa wepesi. Sharti ifuatiliwe kwa dhati. Katika Mpango ambao utaanza Ridvan hii, tunatoa wito ukuaji uchapuzwe katika klasta zote ambazo umeanza. Bila kujali kupwa kwa kawaida na mtiririko wa sifa za mchakato ulio hai, hapo litokee tao dhahiri la maendeleo katika kipindi cha duru ishirini. Juhudi hizi za pamoja sharti zilenge kuinua idadi ya klasta ambapo mpango wa ukuaji umekuwa wenye nguvu hadi kufikia 5,000 mnamo Ridvan 2021.

20. Tunaweka shabaha hii mbele ya ulimwengu wa Kibaha'i tukifahamu kwamba kwa kweli ni ngumu; kwamba kazi yenye kuhitaji nguvu nyingi itahitajika; kwamba dhabihu nyingi lazima zitolewe. Lakini tukikabiliwa na hali mbaya ya ulimwengu ambao huteseka zaidi kila siku ukinyimwa kiowevu cha Baha'u'llah, hatuwezi, kwa ufahamu huu, kuwaomba kitu chochote

pungufu wafuasi Wake waliojifunga. Mungu ajaliapo, jitihada zao zitathibitika kuwa zistahilizo kuvisha taji miaka mia ya kazi ya sulubu na kuweka hatua kwa ajili ya vitendo vya ujasiri ambavyo bado kuwazika kwamba sharti vipambe karne ya pili ya Zama za Ujenzi.

21. Katika miezi ijayo, mtakuwa mkianzisha ushauriano na Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa kutathmini pamoja nao matokeo ambayo lengo hili la kiulimwengu linayo kwa ajili ya jumuiya zao husika, mchakato wa ushauriano ambao sharti kwa haraka upanuliwe hadi kufikia umma. Utendaji sharti basi ufuate. Tunatarajia kwamba maendeleo yatakuwa yamefikiwa kwa haraka zaidi katika maeneo ambapo mpango mmoja au zaidi ya ukuaji wenye nguvu imedumishwa kwa muda fulani, kwa kuwa hizi hutoa chanzo cha thamani cha elimu na uzoefu na huwakilisha hazina ya rasilimaliwatu kadiri juhudi zifanyikavyo kuimarisha maeneo yazungukayo. Ufuatiliaji wa lengo hili pia utapelekea katika uibukaji wa mipango mipya ya ukuaji, mara nyingi katika klasta ambazo hazijafunguliwa na ambazo ni jirani na zile ambapo maendeleo ya maana yametokea. Mtiririko kama huo wa msaada hupata chanzo chake katika masharti yaliyowekwa katika Nyaraka za Mpango Mtakatifu.

***Ujumuishaji wa idadi kubwa na usimamiaji tata.***

22. Ambapo, wakati mpango wa ukuaji ni mchanga katika klasta, kunaweza kuwepo konzi ya kutosha ya watu ambao hujihusisha katika uendelezaji wake na wale ambao wanashiriki wangeweza kutoka katika kaya kadhaa tu, wakati mpango umekuwa wenye nguvu, tarakimu hizi, kama ambavyo mtu angetarajia, zimeakua: labda makumi ya watu wanaojishughulisha katika kazi ya upanuzi na uimarishaji, wakati wale wanaoshiriki wangezidi mia moja. Lakini ili kuweza kufikia idadi kubwa - uhamasishaji wa watu mia moja au zaidi, ambao huduma yao huwaunganisha na mamia au hata maelfu - huhitaji uwezo wa kukabiliana na ongezeko kubwa katika utata.

23. Kadiri mchakato wa ukuaji uendeleavyo kupata nguvu, juhudi za marafiki kushiriki katika mazungumzo ya maana huwaleta katika nafasi nyingi za kijamii, zikiruhusu upangaji mpana zaidi wa watu kuyafahamu mafundisho na kufikiria kwa dhati mchango wanaoweza kuutoa kwa ajili ya uboreshaji wa jamii. Kwa nyongeza, nyumba nyingi zaidi na zaidi huandaliwa kama mahali pa kukutania kwa ajili ya shughuli za ujengaji jumuiya, zikifanywa kila mojawapo kituo kwa ajili ya utawanyaji wa mwangaza wa mwongozo mtakatifu. Mchakato wa taasisi huja kusaidiwa na idadi iongezekayo ya marafiki wanaohudumia kwa ustadi kama wakufunzi ambao, duru baada ya duru, hutoa mfululizo kamili wa kozi za taasisi kati yao, wakati mwingine kwa nguvu kubwa. Hivyo, ukuzwaji wa rasilimali watu huendelea kwa uingiliwaji mdogo na huzalisha bwawa lipanukalo daima la watenda kazi. Wakati ikiendelea kuchota kwenye makundi mbalimbali ya wakazi wa klasta, wale wanaochukua kozi zake kwa idadi kubwa mno mara nyingi ni vijana. Nguvu ya mabadiliko ya ujifunzaji wa Neno la Mungu huhisiwa na wengi ambao maisha yao huguswa kwa njia fulani na shughuli za juamuiya. Na kadiri mtiririko wa watu waanzao njia ya huduma hutanuka, maendeleo makubwa hufanywa katika nyanja zote za

juhudi za marafiki za ujengaji jumuiya. Wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi na walimu wa madarasa ya watoto huongezeka katika idadi, huchochea upanuzi wa programu hizi mbili muhimu. Watoto huwezeshwa kuendelea kutoka daraja moja la madarasa hadi lingine, wakati ambapo vikundi vya vijana chipukizi huendelea kutoka mwaka hadi mwaka na kuimarisha ujifunzaji wao katika huduma kwa jamii. Mawakala wa klasta wakiungwa mkono kwa msaada wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali, hutia moyo na kukuza njia ya kiasili ya washiriki kutoka hatua moja ya mchakato wa kielimu hadi nyingine. Mfumo wa kielimu pamoja na vipengele vyake vyote, ukiwa na uwezo wa kupanuka kukaribisha idadi kubwa, sasa umeota mizizi imara kabisa ndani ya klasta.

24. Maendeleo ya aina hii huhitaji juhudi za pamoja za marafiki popote pale waishipo katika klasta. Hata hivyo, uzoefu katika Mpango wa hivi sasa huonesha kwamba mtindo wa utendaji ambao una uwezo wa kujumuisha idadi kubwa huja kwa kiasi kikubwa kutoka kwenye ufanyaji kazi kuleta maeneo zaidi ya ujirani na vijiji – mahali ambapo ukutanikaji wa nguvu za kiroho husababisha mabadiliko ya haraka ndani mwa mkusanyiko wa watu – hadi pale ambapo wanaweza kudumisha shughuli ya nguvu. Kiini cha watu binafsi kutoka ndani ya kila mojawapo hujitwalia jukumu kwa ajili ya mchakato wa ujengaji uwezo ndani ya wakazi wake. Sehemu kubwa ya idadi ya watu inashirikishwa katika mazungumzo, na shughuli zinafunguliwa kwa makundi yote mara moja – makundi ya marafiki na majirani, vikosi vya vijana, familia nzima – wakiwezeshwa kutambua jinsi jamii iwazungukayo inavyoweza kuundwa upya. Mazoea ya kukusanyika kwa ajili ya ibada ya pamoja, mara nyingine kwa ajili ya sala za alfajiri, hulea ndani mwa wote muunganisho wa ndani zaidi na Ufunuo wa Baha'u'llah. Mazoea yaliyotapakaa, desturi na namna za kujieleza vyote huwa vyenye kuweza kuathiriwa kirahisi na mabadiliko – udhihirisho wa nje na hata mbadiliko wa ndani zaidi, ukiathiri roho nyingi. Vifungo ambavyo huwaunganisha wote pamoja huwa vyenye upendo zaidi. Sifa za usaidizi wa pamoja, kutendeana, na huduma ya mmoja kwa mwingine huanza kujitokeza kama sura za utamaduni upumao, uibukao miongoni mwa wale wajihusishao katika shughuli. Marafiki katika maeneo kama hayo husaidia mawakala wa klasta kupanua mchakato wa ukuaji kwenye sehemu mbalimbali za klasta kwa kuwa wana shauku kuwajulisha wengine muono wa mbadiliko ambao wao wenyewe tayari wameupata kidogo.

25. Wakati wakiendelea na jitihada zao, waumini hukutana na upokevu ndani ya idadi ya watu wa kipekee ambao huwakilisha vikundi maalum vya kiasili, vya kikabila, au vikundi vingine na ambavyo huweza kuwa wamejikusanya pamoja katika mazingira madogo au wapo sehemu zote ndani ya klasta nzima na hata nje. Kuna mengi ya kujifunza juu ya nguvu ihusikayo wakati idadi ya watu wa aina hii huikubali Imani na huhuishwa kupitia ushawishi wake uadilishao. Tunasisitiza umuhimu wa kazi hii kwa ajili ya uendelezaji wa Hoja ya Mungu: kila watu wana sehemu katika utaratibu wa ulimwengu wa Baha'u'llah, na wote sharti wakusanywe pamoja chini ya bendera ya umoja wa binadamu. Katika hatua zake za mwanzoni, juhudi ya kimpangilio ya kuifikia idadi ya watu na kukuza ushiriki wake katika mchakato wa ujengaji uwezo

hujichapuza kwa uwazi wakati wa idadi hiyo ya watu wao wenyewe wamo katika msitari wa mbele wa juhudi hiyo. Watu hawa watakuwa na umaizi maalum ndani ya nguvu zile na miundo katika jamii zao ambazo zinaweza, katika njia mbalimbali kuimarisha jitihada ziendeleazo.

26. Kadiri ukuaji katika klasta unavyosonga mbele zaidi, mahitaji makubwa zaidi huwekwa kwenye utaratibu wa kimpangilio wa taasisi ya mafunzo. Waratibu wa ziada sasa huhitajika, baadhi yao wanaweza kumakinikia sehemu mojawapo maalum ya klasta. Hata hivyo, hii haihitaji kutoa tabaka lingine la utawala. Mengi yanaweza kutimizwa kupitia ushirikiano, wakati waratibu waanzapo kufanya kazi pamoja katika timu, wakati mwingine wakichota msaada wa watu wengine mmoja mmoja wenye uwezo. Mwingiliano endelevu na ubadilishanaji wa uzoefu ndani ya timu hizi daima huboresha uelewa na huongeza ufanisi wa huduma yao. Waratibu pia hugundua kwamba jitihada zao zinaweza kuzidishwa ikiwa marafiki wanaohudumu kama walimu wa watoto, kama wahuishaji, na kama wakufunzi ambao huishi katika ujirani wa karibu mmoja kwa mwingine wanaweza kukutana katika vikundi vidogo, katika mazingira wanayohudumu, na kusaidiana.

27. Wakati huo huo, Kamati ya Ufundishaji ya Eneo inainukia kwenye kiwango kipya cha utendaji. Inajihusisha katika kuijua kinaganaga zaidi hali katika klasta nzima: kwa upande mmoja, kutathmini kwa usahihi uwezo mbalimbali wa jumuiya na matokeo yatolewayo na ukuaji endelevu, na kwa upande mwingine, kuelewa uhusikaji wa uhalisia mbalimbali wa kijamii kwa ajili ya ujenzi wa jumuiya kwa kipindi kirefu. Katika mipango iiwekayo kwa kila duru, Kamati kwa kiasi kikubwa huwategemea wale ambao hubeba sehemu kubwa mno ya kazi ya upanuzi na uimarishaji, lakini kwa kuzingatia kwamba idadi ya wale waliounganishwa kwa namna fulani na mtindo wa shughuli sasa ni kubwa, maswali mbalimbali hubana zaidi: jinsi gani ya kuhamasisha waumini wote katika kusaidia malengo ya ufundishaji; jinsi gani ya kuandaa ziara za majumbani zenye mpangilio kwa marafiki ambao wangenufaika kutokana na uimarishaji na majadiliano ambayo huwaunganisha na jamii; jinsi gani ya kuimarisha vifungo vya kiroho na wazazi wa watoto na vijana chipukizi; jinsi gani ya kujenga shauku ya wale ambao wameonesha nia njema kwa Imani lakini bado hawajashiriki katika shughuli zake. Kusaidia kuanzishwa kwa haraka kwa ufanyaji wa mikutano ya ibada ni suala lingine, ili kwamba mamia ya watu, hatimaye maelfu, wajishirikishe katika kuabudu kwa uambatanaji wa wana-kaya pamoja na majirani zao. Hatimaye, bila shaka, Kamati hujielekeza katika kuendelea kupanua jitihada za jamii ili kwamba roho zaidi na zaidi ziweze kuufahamu ujumbe wa Baha'u'llah. Katika kusimamia utata wa aina mbalimbali uliopo katika kazi yake – ambayo ni pamoja na ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za kitakwimu, hali kadhalika kazi zinginezo – Kamati huchota usaidizi wa mtu mmoja mmoja mbali na wajumbe wake yenyewe. Utata huu pia huhitaji ushirikiano uongezekao wa karibu na Mabaraza ya Kiroho ya Mahali.

28. Kwa upande wake, na katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya washiriki wa shughuli, Baraza la Kiroho la Mahali hukuza uwezo wake wa kutekeleza majukumu mengi iyabebayo kwa

niaba ya jumuiya ikuayo. Linatafuta kutengeneza mazingira ambamo wote hujisikia kutiwa moyo kuchangia kwenye shughuli ya pamoja ya jumuiya. Ni lenye shauku kuona asasi za klasta zinafanikiwa katika mipango yao na uzoefu wa karibu zaidi na hali katika eneo lake huwezesha kuendeleza maendeleo ya mwingiliano wa michakato katika ngazi ya chini. Likiwa na hili akilini, huwasihi marafiki kushiriki kwa moyo wote katika kampeni na mikutano ya tafakari, na hutoa rasilimali nyenzo na usaidizi mwingine kwa ajili ya ubunifu na matukio yanayoratibiwa katika eneo. Baraza pia lipo makini kwa ajili ya mahitaji ya waumini wapya kulelewa kwa uangalifu kwa kuzingatia lini na kwa kiasi gani ukubwa mbalimbali wa maisha ya jamii unavyotakiwa kutambulishwa kwao. Kwa kuwatia moyo kujihusisha kwao katika kozi za taasisi linakusudia huhakikisha kwamba tangu mwanzo kabisa wanajichukulia wenyewe kama wahusika wakuu wa shughuli bora kabisa za kuujenga upya ulimwengu. Linahakikisha kwamba mikusanyiko kwa ajili ya Karamu ya Siku Kumi na Tisa, maadhimisho ya Siku kuu Takatifu, na chaguzi za Kibaha'i huwa fursa ya kuimarisha maadili ya hali ya juu ya ukamilifu wa jumuiya, huimarisha hisia yake ya ushiriki wa pamoja, na kuimarisha sifa zake za Kiroho. Kadiri idadi katika jumuiya inavyokua kubwa zaidi, Baraza huwaza lini ingefaa kugatua mikutano kama hiyo ili kwamba kuwezesha ushiriki mkubwa daima juu ya fursa hizi muhimu.

29. Sifa bainifu ya klasta zilizoendelea ni mtindo wa ujifunzaji ambao hujipenyeza na kuenea katika jumuiya nzima na kuwa kama kichocheo cha kuinua uwezo wa kiasasi. Maelezo ambayo hutoa umaizi katika njia, mbinu, au mchakato kamili huendelea kutiririkia na kutoka vifuko vya shughuli. Mkutano wa tafakari wa klasta nzima, ambamo ujifunzaji huu mwingi zaidi huwasilishwa, mara nyingi hukamilishwa na mikutano kwa ajili ya maeneo madogo madogo zaidi, ambayo hufanyiza hisia ya nguvu zaidi ya uwajibikaji miongoni mwa wale wanaohudhuria. Hisia hii ya umiliki wa pamoja huwa dhahiri zaidi kutoka duru hadi duru – nguvu itolewayo na muunganiko wa kundi la watu wanaojitwalia jukumu la maendeleo yao ya kiroho juu ya vizazi vijavyo. Na kadiri wafanyavyo hivyo, msaada wapatao kutoka asasi za kanda na za kitaifa za Kibaha'i na mawakala wao hudhihirishwa kama mtiririko wa upendo usio na kikomo.

30. Matokeo ya kiasili ya uibukaji wa yote mawili rasilimali na wa ufahamu wa maana ya Ufunuo kwa ajili ya maisha ya watu ni uamshaji wa shughuli za kijamii. Si mara chache, jitihada za namna hii huibuka kama kiumbe hai kutokana na program ya uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi au hutokana na mashauriano kuhusu hali mahali ambazo zinajitokeza kwenye mikusanyiko ya kijamii. Aina ambazo jitihada kama hizo zinaweza kujitwalia ni za namna anuwai na hujumuisha, kwa mfano, msaada wa ukufunzi kwa watoto, miradi ili kuboresha mazingira ya kimwili, na shughuli za kuboresha afya na kuzuia magonjwa. Baadhi ya jitihada huwa endelevu na pole pole hukua. Katika maeneo mbalimbali uanzishwaji wa shule za jamii katika ngazi za umma umeibuka kutokana na mahitaji ya hali ya juu kwa ajili ya elimu ifaayo ya watoto na ufahamu wa umuhimu wake, ukibubujika kwa asili kutokana na ujifunzaji wa nyenzo za taasisi. Inapobidi, jitihada za marafiki kwa kiwango kikubwa zinaweza kuimarishwa kupitia

kazi ya shirika linalofuata mwongozo wa Ki-Baha'i lililoanzishwa likifanya kazi katika maeneo ya karibu. Japokuwa duni kiasi gani shughuli za kijamii mwanzoni zaweza kuwa, ni ishara ya watu wakuzao ndani mwao wenyewe uwezo muhimu mkuu kabisa, ule ushikiliao uwezo wa ndani usio na kikomo na umuhimu kwa ajili ya karne zijazo: kujifunza namna ya kutumia Ufunuo katika viwango vya aina mbalimbali vya maisha ya kijamii. Jitihada zote kama hizo pia husaidia kuboresha ushiriki, katika ngazi ya mtu mmoja mmoja na wa pamoja, katika mijadala iliyoenea ya jamii pana zaidi. Kama ilivyotarajiwa, marafiki wanaletwa zaidi kwenye maisha ya jamii – maendeleo ambayo ni ya asili katika mtindo wa utendaji katika klasta tangu mwanzoni kabisa, lakini ambao sasa ni wazi zaidi.

31. Hadi mjongeo wa idadi ya watu kufikia hapa huonesha kwamba mchakato ambao umeileta una nguvu ya kutosha kutimiza na kudumisha kiwango cha juu cha ushiriki katika nyanja zote za jitihada za ujengaji uwezo na kusimamia utata uliopo. Hii ni hatua nyingine ya ukuaji kwa ajili ya marafiki kuipita, ya tatu kwa mfuatano tangu mchakato wa ukuaji katika klasta ulipoanzishwa. Huashiria utokeaji wa mfumo kwa ajili ya upanuzi, katika kituo hadi kituo, mtindo wenye nguvu wa maisha ya jamii ambao unaweza kuwashirikisha watu – wanaume kwa wanawake, vijana kwa watu wazima – katika kazi ya mabadiliko yao wenyewe ya kiroho na kijamii. Hii tayari imetokea katika takribani klasta mia mbili, ikijumuisha hali ya kijamii na kiuchumi, na tunatumaini kwamba, hadi mwishoni mwa Mpango ujao, itaonekana katika klasta mia kadhaa zaidi. Ni hatima ambayo kwayo marafiki wafanyao kazi katika maelfu ya klasta kwingineko ulimwenguni wanaweza kuiwekea lengo.

32. Katika baadhi ya klasta ambako ukuaji umepiga hatua hadi kwenye kiwango hiki, maendeleo ya kusisimua zaidi yametokea. Kuna maeneo ndani ya klasta hizi ambako asilimia ya kutosha ya idadi nzima ya watu hivi sasa inajihusisha na shughuli za ujenzi wa jumuiya. Mathalani, kuna vijiji vidogo ambako taasisi imeweza kuhusisha na ushiriki wa watoto wote na vijana chipukizi katika programu zake. Wakati ueneaji wa shughuli umekuwa mkubwa, matokeo ya kijamii yatokanayo na Imani huwa dhahiri zaidi. Jumuiya ya Kibaha'i husimama daraja la juu zaidi kama sauti ya kipekee ya uadilifu katika maisha ya watu na inaweza kuchangia mtazamo uliojulishwa kwenye mijadala inayoizunguka, tuseme, maendeleo ya vizazi vichanga. Wenye mamlaka kutoka jamii pana wanaanza kuchota umaizi na uzoefu uibukao kutoka jitihada za shughuli za kijamii zilizovuviwa na mafundisho ya Baha'u'llah. Mazungumzo yanayoshawishiwa na mafundisho hayo, yahusuyo usitawi wa watu wote, hupenyeza na kuenea sehemu pana zaidi ya idadi ya watu, hadi kufikia mahali ambako matokeo ya juu ya mjadala mzima katika eneo yanaweza kutambulika. Mbali na jamii ya Kibaha'i, watu wanaliona Baraza la Kiroho la Mahali kama chanzo angavu cha hekima ambacho kwacho wao vile vile wanaweza kukigeukia kwa ajili ya uangazio.

33. Tunatambua kwamba maendeleo kama haya bado ni matarajio ya mbali kwa klasta nyingi, hata zile ambamo mtindo wa shughuli hujumuisha idadi kubwa. Lakini katika baadhi ya maeneo,

hii ni kazi ya wakati huu. Katika klasta kama hizo, wakati marafiki wakiendelea kujishughulisha na kudumisha mchakato wa ukuaji, vipimo vingine vya jitihada za Kibaha'i huhitaji sehemu iongezekayo ya umakini wao. Wanatafuta kuelewa jinsi gani kushamiri kwa jamii ya wenyeji kunavyoweza kubadili jamii ambayo kwayo yenyewe ni sehemu yake. Huu utakuwa ni wigo mpya wa ujifunzaji kwa ajili ya maono ya siku zijazo, ambako umaizi utafanyizwa ambao hatimaye utaunufaisha ulimwengu mzima wa Ki-Baha'i.

*Uachiliaji wa uwezo wa vijana*

34. Ujasiri wa ajabu wa vijana katika uwanja wa huduma ni mojawapo ya matunda bora kabisa ya Mpango wa sasa. Kama uthibitisho wowote ulihitajika wa uwezo usio wa kawaida ambao vijana wanao, umetolewa bila kubishaniwa. Katika uamshaji uliotokana na makongamano ya vijana yaliyoitishwa mwaka 2013, nguvu iliyosambaa ambayo iliwekwa kwa kazi inayoendelea ndani ya klasta huonesha dhahiri jinsi jumuiya ya Jina Kuu Kabisa ilivyo na uwezo wa kuleta sura ya hali ya juu kabisa ya matamanio ya vijana. Ni kwa namna gani tumefurahishwa kuona kwamba, kufuatana na ushiriki wa zaidi ya vijana 80,000 katika makongamano haya, ongezeko la wana-rika zaidi ya 100,000 wameungana nao kushiriki katika mikutano mingi tangu kipindi hicho. Hatua kwa ajili ya utiaji moyo ujihusishaji kamilifu wa idadi hizi zikuazo katika shughuli za jumuiya lazima ziwe sehemu kubwa ya Mpango mpya.

35. Ushiriki wenye shauku wa vijana pia ulisisitizia ukweli kwamba wanawakilisha kipengele cha mwitikio mkubwa kabisa wa uwajibikaji wa kila kundi kubwa la watu wapokevu ambao marafiki wamechagua kuwafikia. Ujifunzaji uliopatikana katika mintarafu hii ni jinsi ya kuwasaidia vijana kuwa na ufahamu wa mchango wanaoweza kuutoa ili kuboresha jamii zao. Kadiri ufahamu uamshwavyo, wanajifunganisha na malengo ya jumuiya ya Ki-Baha'i na wanaonesha hamu ya kusaidia nguvu zao kwa kazi inayoendelea. Mazungumzo katika hali hizi huwasha nia ya jinsi gani nguvu za kimwili na kiroho zinazopatikana kwao katika muda huu wa maisha zinavyoweza kuelekezwa kwenye utoaji wa mahitaji ya wengine, hususani kizazi kichanga zaidi. Mikusanyiko maalum ya vijana, inayofanyika mara kwa mara hivi sasa katika ngazi ya klasta na hata ujirani au kijiji, imethibitisha kuwa fursa bora kwa ajili ya kuleta nguvu kwa mazungumzo haya yanayoendelea, na zinaongezeka kuwa sehemu muhimu ya pamoja ya duru za shughuli katika klasta nyingi.

36. Uzoefu hupendekeza kwamba mjadala kuhusu uchangiaji kwenye uboreshaji wa jamii hushindwa kuchota kwenye chemchemi yenye vina virefu kabisa vya motisha endapo utaacha uchunguzi wa mawazo ya kiroho. Umuhimu wa "kutenda", wa kuinuka kuhudumu na kuambatana na roho wenzi, lazima vipatanishwe na dhana ya "kuwa", wa kuongeza uelewa wa mtu wa mafundisho matakatifu na kuakisi nje sifa za kiroho katika maisha ya mtu. Na kwa hivyo ni kwamba, baada ya kutambulishwa kwenye muono wa Imani kwa binadamu na tabia za enzi ya ujumbe wake, vijana huhisi kiasilia hamu ya kuwa watoa huduma, hamu ambayo taasisi za mafunzo huiitikia kwa haraka. Kwa hakika, uachiliaji wa uwezo wa vijana ni wajibu mtakatifu

kwa kila taasisi ya mafunzo. Bado ukuzaji wa uwezo huo kadiri uendeleavyo ni wajibu wa kila asasi ya Hoja. Utayari ambao vijana huuonesha kwenye uchukuaji wa hatua, katika uwanda wowote wa utendaji wauchaguao, unaweza kuzuia ukweli kwamba wanahitaji msaada endelevu kutoka asasi na mawakala katika klasta mbali zaidi ya hatua za mwanzoni.

37. Vijana pia husaidiana mmoja kwa mwingine katika mintarafi hii, wakija pamoja katika makundi kujihusisha katika ujifunzaji zaidi na hujadili huduma yao, kuimarisha juhudi za mmoja kwa mwingine na kujenga azma, wakitazamia ya kupanua daima duara la urafiki kwa upana zaidi. Utiaji moyo utolewao kwa njia hii na mtandao wa wenzi-rika huwapa vijana njia mbadala ihitajikao zaidi – sana kwa zile sauti za kushawishi ambazo huwaalika kwenye vishawishi vya kimatumizi na bughudha zisizoweza kuzuilika, hali kadhalika upinzani kwenye miito ya kukatili wengine. Ni dhidi ya ongezeko la udhoofishaji wa anasa na ugawanyikaji wa jamii ambavyo program ya vijana chipukizi hudhihirisha thamani yake mahsusi katika muda huu. Huwapa vijana uwanja bora ambamo huwasaidia wale ambao ni wadogo zaidi yao kuhimili nguvu haribifu ambazo hasa huwalenga wao.

38. Kadiri vijana waendeleavyo katika njia ya huduma, jitihada zao hujumuishwa bila kukatishwa kwenye shughuli za klasta, na kama matokeo, jumuiya nzima huneemeka kama kitu kimoja kilichoshikamana. Kuzifikia familia za vijana ni njia asilia ya kuimarisha ujenzi wa jumuiya. Asasi na mawakala wamepewa changamoto ya kuongeza uwezo wao binafsi ili kutafuta njia za utaratibu wa utambuzi wa uwezo wa vijana. Kwa kuwa na ufahamu mkubwa zaidi wa hali na mienendo ya kundi-rika hili wanakuwa na uwezo wa kupanga ipasavyo – mathalani, kutoa fursa kwa ajili ya vijana kujifunza kozi kwa nguvu, pengine haraka iwezekanavyo baada ya kuhitimisha kusanyiko la vijana. Ujazaji wa nguvu kutoka kundi la vijana lipumalo huruhusu kuchochea mwendo wa kazi ndani ya klasta kuchapuzwa.

39. Wakati ni vyema kutarajia mambo makubwa kutoka kwa wale walio na mengi ya kutoa katika njia ya huduma, marafiki lazima wajihadhari dhidi ya kujitwalia na kutumia mtazamo finyu juu ya nini maendeleo kuelekea ukomavu uhitaji. Uhuru wa mjongeo na upatikanaji wa muda huwawezesha vijana wengi kuhudumu katika njia ambazo moja kwa moja huendana na mahitaji ya jumuiya, lakini kadiri wasongavyo mbele zaidi kwenye miaka yao ya ishirini, upeo wao hupanuka. Vipimo vingine vya maisha yaliyoshikamana, vinavyodai sawia na vyenye ustahilivu wa hali ya juu, huanza kufanya madai ya nguvu zaidi juu ya umakini wao. Kwa wengi, kipaumbele cha haraka kitakuwa elimu zaidi, taaluma au ufundi, kutokana na uwezekano uliopo mbele yao, na nafasi mpya kwa ajili ya mwingiliano na jamii hufunguka. Zaidi ya hayo, vijana wa kike na kiume huwa na ufahamu mkali wa nasaha za Kalamu Kuu kabisa "waingie katika ndoa" kwamba waweze "kumzaa yule atakayelitaja Jina Langu miongoni mwa watumishi Wangu" na "kujishughulisha katika kazi za mikono na taaluma." Baada ya kupata kazi, kwa kawaida vijana hujaribu kuchangia kwenye uwanja wa taaluma zao au hata kuiendeleza katika mwanga wa umaizi wanaoupata kutokana na kuendelea kwao kujifunza Ufunuo, na wanajibidiisha kuwa mifano ya uadilifu na ubora katika kazi zao. Bahá'u'lláh huwatukuza sana

“wale wajipatiao riziki kwa kazi zao na kutumia juu yao wenyewe na juu ya ndugu zao kwa upendo wa Mungu, Bwana wa malimwengu yote.” Kizazi hiki cha vijana kitaunda familia ambayo itadumisha misingi ya jamii inayositawi. Kupitia upendo wao ukuao kwa Bahá’u’lláh na msimamo binafsi kwa kiwango ambacho Yeye huwashauri wao watoto wao watajifunza upendo wa Mungu, “wakichanganya na maziwa ya mama zao”, na mara zote wakitafuta hifadhi ya sheria Zake takatifu. Kwa udhahiri, basi, wajibu wa jumuiya ya Ki-Baha’i kwa vijana hauishii pale wanapoanza kwanza huduma. Maamuzi muhimu wayafanyayo kuhusu muelekeo wa maisha yao ya utu uzima yataamua iwapo huduma kwenye Hoja ya Mungu ilikuwa ya muda mfupi tu na sura ya kukumbukwa ya miaka yao ya ujana, au kituo cha kudumu cha uwepo wao duniani, kioo ambacho kupitia humo matendo yote hulengwa. Tunawategemea ninyi na wasaidizi wenu kuhakikisha kuwa matarajio ya kiroho na ya kimwili ya vijana yanapewa uzito unaostahili katika majadiliano ya familia, jumuiya, mawakala, na asasi.

***Kuongeza Uwezo wa Kiasasi***

40. Mahitaji ya Mpango wa sasa – kuanzisha maelfu ya program mpya za ukuaji na kuimarisha zilizopo – yalihitaji kutoka asasi za kitaifa na kikanda, hali kadhalika na ninyi wenyewe, ujasiri imara na uratibu. Utimizwaji wake uliwezekana kupitia moyo wa pamoja wa ushirikiano baina ya wahusika wakuu watatu wa Mpango – mtu binafsi, jumuiya na asasi. Moyo huu ulikuwa sharti kwa kila shughuli muhimu, ikijumuisha jitihada maalum ya kuwafanyia makazi watangulizi katika nchi zilizochaguliwa na, bila shaka, uandaaji wa makongamano 114 ya vijana. Mwelekeo ulioeneo wa huduma yenye furaha, unyumbulifu, na kujitenga kutoka upendeleo binafsi vilizipa hata shughuli za kila siku za kiutawala ubora mtakatifu. Mahitaji mapya ya Mpango ujao bila shaka, yataendelea zaidi kupima uwezo wa asasi za Ki-Baha’i, lakini bila kujali chochote, hakika yataendelea kuhifadhi moyo huu wa umoja miongoni mwa wote wanaotenda kazi pamoja.

41. Kama ilivyooneshwa hapo awali, mjongeo wa klasta katika mwendeleo hutegemea uwepo wa uwajibikaji kutoka kwa asasi ili kuongoza na kusaidia mawakala wa klasta na kuwapa rasilimali kadiri zihitajikavyo. Kazi hii ni wajibu wa kimsingi wa Halmashauri za Ki-Baha’i za Kanda na taasisi za mafunzo za kanda. Idadi ya Halmashauri ulimwenguni ilipanda kutoka 170 hadi 203 katika miaka mitano iliyopita, ikiasi hitaji likualo na uwezo uongezekao kwa kazi inayotakiwa kufanywa katika kiwango hiki, na katika baadhi ya nchi ambako Halmashauri bado hazijaundwa, hatua mahsusi zilichukuliwa kujenga uzoefu katika matarajio ya uibukaji wao, kama vile uteuzi wa timu za kanda. Katika baadhi ya kanda ambazo zimechukua eneo kubwa la nchi, Halmashauri zimeweka mipangilio kwa ajili ya kulea maendeleo ya makundi ya klasta zinazokaribiana. Wakati huo huo, katika nchi ndogo ambazo hazihitaji uanzishwaji wa Halmashauri za Kanda, Mabaraza ya Kitaifa yanaendelea kutoa mawazo kwenye njia za kusaidia klasta kuendelea, katika mazingira fulani kwa kuunda kundi lililopewa kazi hii; mnatiwa moyo kuchochea ujifunzaji katika eneo hili, kwa shabaha kwamba, kwa wakati upasao miundo rasmi inaweza kufafanuliwa ambayo itachukua wajibu huu kama ambavyo Halmashauri zifanyavyo

kazi katika nchi zingine. Na, kama ilivyo kwa Halmashauri, tunatazamia kwamba muundo wowote utakaoibuka katika ngazi ya kitaifa utanufaika kutokana na mwingiliano na Asasi ya Washauri.

42. Ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, asasi za kanda na kitaifa zitahitaji kujifahamisha kikamilifu juu ya maendeleo kwenye ngazi ya umma na nini wanajifunza katika klasta ambazo maendeleo yake wanayasimamia. Upatikanaji wa taarifa kwa wakati kuhusu mjongeo wa klasta na kazi ya taasisi ndani ya mamlaka yao unahitajika kwa ajili ya asasi kusaidia mawakala wao na kuchukua maamuzi husika, mathalani, upelekaji wa watangulizi, mgawanyo wa fedha, kuandaa na kukuza vitabu vya Ki-Baha'i, na upangaji wa mikutano ya kiasasi; huwaruhusu kuusoma uhalisia wa jumuiya zao kwa usahihi na kutenda kwa msingi wa mahitaji yanayoeleweka wazi wazi wanapoelekeza nguvu za marafiki katika kufanikisha mahitaji ya haraka ya saa. Katika hatua mbali mbali Baraza la Kitaifa, kwa kushauriana nanyi, wanaweza kuona ni vema kuchukua na kusambaza rasmi baadhi ya vipengele vya mafunzo yaliyopatikana, hasa kuhusiana na mfumo wa usimamizi katika ngazi ya klasta na kanda. Haja ya kuwa waliohabarishwa vyema kuhusu uzoefu wa jumuiya unaojilimbikiza hubeba maana mahsusi kwa Mabaraza ya Kitaifa katika nchi kubwa ambazo zina Halmashauri za Kanda kadhaa, hasa pale ambapo Baraza litakuwa limekasimu kwa Halmashauri kazi ya kusimamia taasisi. Hapa, mipangilio mipya katika ngazi ya kitaifa wakati mwingine imekuwa muhimu ili kulipatia Baraza uchambuzi wa maana wa nini kilichopatikana kama funzo katika kanda zote.

43. Bila shaka, Baraza la Kiroho la Kitaifa hatimaye lina jukumu la kukuza nyanja zote za maendeleo ya jumuiya ya Kibaha'i. Ingawa hufuatilia njia mbalimbali za utendaji lenyewe, kwa namna nyingi linatimiza jukumu hili kwa kuhakikisha kwamba Halmashauri za Kanda au mawakala maalum wana uwezo wa kuchukua hatua kuendeleza maeneo ya jitihada waliyokabidhiwa. Kadiri uwezo wa marafiki uongezekavyo na ukubwa wa jumuiya ukuavyo, kazi ya Baraza la Kitaifa katika upana wake huwa tata zaidi. Kwa hiyo, na kwa mujibu wa ukubwa wa kazi zilizo mbele ya asasi katika Mpango ujao, Mabaraza ya Kitaifa – hali kadhalika Halmashauri – zitanufaika kutoka uzingatiaji wa kipindi hadi kipindi, kwa kushirikiana nanyi, ikiwa katika utendaji wao wa kiutawala, na kwa kweli katika vipengele vya utendaji wao wenyewe, vingeweza kurekebishwa au kuongezwa kwa jinsi ambayo ingefaa zaidi kusaidia mchakato wa ukuaji.

44. Kufikia kiwango cha juu zaidi cha kiutendaji vivyo hivyo ni jambo lenye kubana mno la taasisi za mafunzo. Jitihada za jumuiya kuimarisha program za ukuaji katika maelfu ya klasta na kuendeleza utiaji nguvu wao utaweka mahitaji mazito kwa mawakala hawa. Ulengaji wao, bila shaka, ni ukunjukaji wa hatua tatu za mchakato wa kielimu wanaousimamia na uimarishaji wa mchakato wa ujifunzaji uhusikao na kila mojawapo, ili kwamba vyote viwili ubora wa shughuli za taasisi na uwezo wa kuzipanua kwa idadi zikuazo daima vinapanda bila kukoma. Wakati ni muhimu kwamba taasisi zishughulikie masuala ya kiuendeshaji wa siku hadi siku, kiwango cha

kile kinachohitajika kutimizwa huhitaji kwamba pia zijishughulishe na ufikiriaji wa mkakati. Bodi za taasisi ya mafunzo zinahitaji kudumisha ushauriano uendeleao na waratibu wa kitaifa au kanda, hali kadhalika na Washauri Wasaidizi, kuhusu jinsi gani shughuli katika klasta hupata nguvu, jinsi gani zinavyoweza kupewa rasilimali kwa namna inayokidhi, mbinu gani huthibitika kuwa fanisi katika mazingira tofauti tofauti, na jinsi gani uzoefu unaweza kushirikishwa. Akilini mwetu tuna jitihada makini na zenye utaratibu kwa kundi hili linaloshirikiana ili kukusanya na kutumia umaizi uibukao kutoka ngazi ya umma kuhusu uendelezaji wa madarasa ya watoto, vikundi vya vijana chipukizi, na mafunzo ya mzunguko. Kushughulikia maeneo mengineyo ya kazi za taasisi – kama vile taratibu za uratibu katika ngazi ya klasta, kuongeza uwezo wa waratibu, na usimamizi wa takwimu na fedha – kutakuwa muhimu pia. Katika kufanya kazi kwenu pamoja na taasisi za mafunzo, bila shaka mtapenda kupanga kwamba wajifunze kutoka uzoefu wa taasisi zingine katika eneo lile lile la ulimwengu. Maeneo kwa ajili ya utawanyaji wa ujifunzaji kuhusu program za vijana chipukizi pia hutoa chanzo kizuri cha umaizi kwa ajili ya taasisi za nchi jirani au kanda.

45. Kadiri asasi na mawakala wanavyotafuta kuchapuza michakato ya upanuzi na uimarishaji katika kila nchi, suala la rasilimali fedha kwa hakika litahitaji kupewa umakini uongezekao. Kwa kweli, kipengele muhimu cha kuongeza uwezo wa asasi kwa miaka ijayo kitakuwa ni uendelezaji unaoendelea wa Mifuko ya mahali na ya kitaifa. Ili hili litokee, marafiki kwa ujumla wao lazima waalikwe kufikiria upya jukumu la waumini wote kusaidia kazi ya Imani kwa njia zao wenyewe na, zaidi, kusimamia masuala yao ya kifedha kwa mujibu wa mafundisho.

46. Ustaarabu wa siku zijazo uliotazamiwa na Baha'u'llah ni wenye neema, ambamo rasilimali nyingi za ulimwengu zitaelekezwa kwenye uinuaji na wongofu wa binadamu, si kwenye udhalilishwaji wake na uharibifu. Kitendo cha uchangiaji kwenye Mfuko, basi, kimejaliwa maana ya ndani sana: ni njia ya kivitendo ya uharakishaji wa ujio wa ustaarabu huo, na cha lazima, kwa kuwa kama Baha'u'llah Mwenyewe alivyoelezea, "Yeye Ambaye ndiye Ukweli wa Milele – utukuzwe utukufu Wake – amefanya utimizwaji wa kila jitihada duniani kutegemea juu ya njia za kimwili." Wa-Baha'i huendesha maisha yao katikati ya jamii iliyovurugika vikali katika mambo yake ya kimwili. Mchakato wa ujenzi wa jumuiya wanaouendeleza katika klasta zao hukuza idadi ya mitazamo kuelekea utajiri na mali ambavyo ni tofauti kabisa kutoka ile inayoshikiliwa na myumbo ulimwenguni. Tabia ya kutoa mara kwa mara kwenye Mfuko wa Imani – ikiwemo michango ya vitu hasa katika maeneo fulani fulani – huinuka kutoka na huendeleza hali ya matakwa ya mtu binafsi kwa ustawi wa jumuiya na maendeleo ya Hoja. Wajibu wa kuchangia, kama ulivyo wajibu wa kufundisha, ni kipengele cha msingi cha utambulisho wa Ki-Baha'i ambacho huimarisha imani. Michango ya kujihini na ya ukarimu ya muumini mmoja mmoja, ufahamu wa pamoja wa mahitaji ya Mfuko unaojengwa na jumuiya, na ukadamu makini wa rasilimali fedha unaofanywa na asasi za Imani unaweza kufikiriwa kama uonesho wa upendo ambao huwafungamanisha pamoja kwa ukaribu zaidi watendaji hawa watatu. Na hatimaye, utoaji wa hiari hukuza ufahamu kwamba usimamizi wa masuala ya kifedha

wa mtu binafsi kwa mujibu wa kanuni za kiroho ni kipimo cha lazima cha maisha yaliyoishi kwa kufungamana. Ni suala la ufahamu, ni njia ambamo kujidhatiti kwenye uboreshaji wa ulimwengu hutafsiriwa katika vitendo.

47. Tunayaelekeza matamko haya kwenu, tukitambua jukumu la kipekee mlilonalo, manaibu wenu, na mabegani mwa wasaidizi wao katika kuwasaidia marafiki kuendeleza uelewa wao katika maeneo mbalimbali, si haba, bila shaka, kwa kufuatana na mbinu mbalimbali za ukuaji. Kama tulivyoonesha hapo awali, katika asasi ya Washauri jumuiya ya Kibaha'i ina mfumo ambao kupitia humo masomo yaliyopatikana katika maeneo ya mbali kabisa ya sayari unaweza kuunufaisha mchakato wa kiulimwengu wa ujifunzaji ambamo kila mfuasi wa Baha'u'llah anaweza kushiriki. Kadiri uelewa endelevu wa kina wa Mpango wa Miaka Mitano uibukavyo miongoni mwa waumini baada ya muda, umaizi unaojitokeza kutokana na utumiaji wa mwongozo hutambuliwa, huelezwa kwa ufasaha, hufyonzwa na hushirikiana. Katika muntarafu huu, jumuiya ya Jina Kuu Kabisa ina deni kubwa la shukrani kwa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, ambacho kimefanya mengi katika miaka ya hivi karibuni, kwa umakini huo, kwa upendo kulea na kwa bidii kueneza mtindo wa ujifunzaji ambao sasa umeimarishwa vyema.

48. Vipengele muhimu vya Mpango ujao, kama vile vilivyokuja kabla yake, vipo bayana. Walakini, uelewa wa kina kabisa wa sehemu zake mbalimbali huhitaji utambuzi wa idadi ya njia za uendeshaji zenye utata wa hali ya juu ambazo kwazo klasta huendelea. Tunaitegemea asasi yenu ikiwa na ufahamu wa kina wa muongozo uhusikao ambao marafiki kwa jumla, na hasa asasi pamoja na mawakala wao, wanaweza kuwategemea ninyi kuyaangazia mashauriano yao kwa kumakinikia kwenye uzingatiaji unaofaa. Ni dhahiri, hata hivyo, haja ya kuwasaidia marafiki katika angalau klasta 5,000 ambako mtindo wa utendaji unaotiwa nguvu itakuwa ni changamoto kubwa, yenye matokeo kwa mtindo wenu wenyewe wa utendaji – lakini hasa zaidi kwa ule wa Washauri Wasaidizi. Klasta ambazo zipo kwenye safu za mbele za mchakato wa ukuaji katika maeneo yao bila kuepukika zitadai sehemu kubwa zaidi ya muda wao; pia, mipangilio ya kiutawala kwenye ngazi ya kanda mara kwa mara itahitaji usaidizi wao. Wanajishughulisha zaidi na kile kitokeacho katika jumuiya; wakiwa makini kwa vyote viwili kwenye maendeleo ya kila hatua ya mchakato wa kielimu na kwenye uimarishaji wa duru za shughuli, wanakuza upatano miongoni mwa njia za utendaji zinazoendelezwa katika klasta na hupepea shauku ya ufundishaji kuwa mwale wa moto. Katika utekelezaji wa jukumu lao la kuendeleza ujifunzaji na kuwasaidia marafiki kuingia katika uwanja wa huduma, wanachota kwa wingi kwenye taasisi ya mafunzo, vipengele ambavyo kazi yake huendana kwa karibu na yao. Lakini majukumu yao mengine hudai vile vile. Hivyo, watahitaji kufikiria jinsi, ili kutimiza yale majukumu makubwa, wanavyoweza kuchota kwa wingi zaidi na kiubunifu zaidi msaada kutoka kwa wasaidizi wao. Wasaidizi, bila shaka, wanaweza kupewa kazi yoyote – rahisi au tata, ya jumla au yenye umaalum wa hali ya juu – na namna hii mbalimbali hufanya uwezo wa kipekee. Wakati baadhi ya wasaidizi wanaweza kujishughulisha na maendeleo ya jumuiya ya mahali, wengine wanaweza kupewa kazi ambazo huhusiana na klasta nzima. Kwa kuwaandaa ipasavyo,

kuwaongoza kadiri uwezo upanukavyo, na pole pole kuongeza majukumu yao, Washauri Wasaidizi wataweza kutumia vyema zaidi uwezekano uliopo. Mengi kwa hakika ni ya kujifunza kama matokeo, na mnatiwa moyo kupata umaizi kutoka uzoefu wa wasaidizi wenu.

***Kipindi chenye nguvu maalum***

49. Ufuatiliaji wa kimpangilio wa Mpango katika vipimo vyake vyote hupelekea kuibuka kwa mwelekeo wa jitihada ya pamoja unaojitofautisha siyo tu kwenye kujifunga kwa ajili ya huduma, lakini pia kwa mvuto wake kwenye ibada. Uzidishwaji wa shughuli ambao miaka mitano inayofuata huhitaji utasitawisha zaidi maisha ya ibada kwa wale wanaohudumu bega kwa bega ndani ya klasta duniani kote. Mchakato huu wa usitawishaji tayari umeendelea zaidi: shuhudieni, mathalani, jinsi mikusanyiko ya ibada ilivyojifungamanisha katika kiini cha maisha ya jumuiya. Mikutano ya ibada ni fursa ambazo roho yoyote inaweza kushiriki, ikivuta pumzi ya manukato ya mbinguni, ikijipatia utamu wa sala, ikitafakari juu ya Neno la Uumbaji, ikisafirishwa kwenye mbawa za roho, na ikizungumza na Mmoja Apendwaye kabisa. Hisia ya urafiki na kusudi la pamoja hufanyizwa, hasa katika mazungumzo ya hali ya juu ya kiroho ambayo kiasili hutokea katika nyakati hizo na kupitia humo “mji wa moyo wa binadamu” unaweza kufunguliwa. Kwa kuitisha mkusanyiko kwa ajili ya ibada ambapo watu wazima na watoto wa kila asili wanakaribishwa, roho ya Mashriqu’l-Adhkar inaamshwa katika mahali popote. Uzidishwaji wa tabia ya ibada ya jumuiya pia una athari kwenye Karamu ya Siku Kumi na Tisa na huweza kuhisiwa nyakati zingine marafiki wanapokusanyika pamoja.

50. Uadhimishwaji wa Siku Takatifu una nafasi maalum katika muntarafu huu. Nyaraka zighaniwazo, na sala, hadithi, nyimbo, na maono yatolewayo – yote hayo ni vielelezo vya upendo kwa wale Watakatifu ambao maisha na ujumbe wao hukumbukwa – hutikisa moyo na hujaza roho kwa kicho na mshangao. Wakati wa Mpango wa Miaka Mitano unaokaribia kuanza, kutatokea matukio ya maana sana ya namna hii: maadhimisho ya miaka – mia — mbili ya Kuzaliwa kwa Bahá’u’lláh na Kuzaliwa kwa Báb mnamo mwaka 2017 na 2019 mtawalia. Sherehe hizi tukufu zitakuwa ni fursa kwa Wa-Baha’i katika kila nchi kuvutia kadiri iwezekanavyo idadi kubwa kabisa ya waumini, familia zao, marafiki, na washiriki, hali kadhalika wengine kutoka jamii pana, kuadhimisha vipindi ambavyo Kiumbe asiye na mwenzi katika uumbaji, Mdhihirishaji wa Mungu, alizaliwa kwa ajili ya ulimwengu. Usherehekeaji wa Siku kuu hizi za kuadhimisha miaka mia mbili kwa hakika utaongeza utambuzi wa jinsi gani uadhimishaji wa Siku Takatifu, sasa kwa mujibu wa kalenda ambayo huwaunganish marafiki wa Mungu kila mahali, huimarisha utambulisho wa Ki- Baha’i.

51. Katika miaka ijayo, jumuiya, kwa hakika, itakutana na mlolongo wa maadhimisho, ukihitimishwa na Siku Kuu ya Maadhimisho ya Miaka Mia Moja ya Kupaa kwa ‘Abdu’l-Bahá mnamo Novemba 2021, ambayo yatafunga karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi. Mwaka ujao Ulimwengu wa Ki-Baha’i utaweka alama ya miaka mia moja tangu Nyaraka za kwanza za

Mpango Mtakatifu zilipobubujika kutoka kalamu ya Bwana. Katika Nyaraka hizi kumi na nne, zilizofunuliwa wakati wa mojawapo ya saa za giza kuu kabisa za binadamu, ‘Abdu’l-Bahá aliweka hati kwa ajili ya kazi ya ufundishaji ambayo ilieleza bayana uwanja wa utendaji wake kuwa sayari nzima. Ikizuiliwa kutumika mpaka mwaka 1937, wakati ambapo wa kwanza katika mfuatano wa Mipango ulipozinduliwa kwa uchochezi wa Mlezi kwa ajili ya Wa-Baha’i wa Marekani ya Kaskazini, Mpango Mtakatifu umeendelea kukunjuka kwa miongo kadiri uwezo wa pamoja wa wafuasi wa Bahá’u’lláh ulivyokua, ukiwawezesha kujitwalia changamoto kubwa zaidi – daima. Ni muono wa ajabu ulioje kwa Mwanzilishi wa Mpango! Akiweka mbele ya marafiki matarajio ya siku wakati mwanga wa ufunuo wa Baba Yake utakapoangaza kila pembe ya ulimwengu, aliweka siyo tu mikakati kwa ajili ya kufanikisha jambo hili kubwa, bali kanuni za kuongoza na mahitaji ya kiroho yasiyobadilika. Kila juhudi iliyofanywa na marafiki kueneza mafundisho matakatifu kwa utaratibu hufuatilia chimbuko lake kwenye nguvu zilizotiwa mwendo katika Mpango Mtakatifu.

52. Jitihada zijazo za ulimwengu ambazo kwazo marafiki wataitwa huhitaji utumiaji wa mikakati iliyothibitishwa, vitendo vya kiutaratibu, uchambuzi wa kiuweledi, na umaizi makini. Bado juu ya yote, ni shughuli ya kiroho, na sifa yake bainifu kamwe haipaswi kutiwa giza. Uharaka wa kutenda unasukumwa na hali ya ukataji tamaa ya dunia. Mambo yote ambayo wafuasi wa Bahá’u’lláh wamejifunza katika miaka ishirini iliyopita lazima yafikie kilele katika utimizwaji wa miaka mitano ijayo. Kipimo cha kile wanachoombwa huleta akilini mojawapo ya Nyaraka Zake ambamo Yeye hueleza kwa maneno yanayochoma, changamoto ya lazima katika uenezaji wa Hoja Yake:

> Ni kiasi gani cha ardhi kimebaki bila kulimwa na kupandwa; na ni ardhi kiasi gani ililimwa na kupandwa, na bado ilibaki bila maji; na ni ardhi kiasi gani ambayo, wakati wa kuvuna ulipofika, hakuna mvunaji aliyejitokeza kuvuna! Hata hivyo, kupitia upendeleo wa maajabu ya Mungu na aya za wema Wake – wa upendo Tunaweka matumaini kwamba roho zitaweza kujitokeza ambazo ni mfano halisi wa njema za mbinguni na ambazo zitajishughulisha na mafundisho ya Hoja ya Mungu na kuwafundisha wote waishio duniani.

53. Jitihada za kiutaratibu za wapendwaWake kote ulimwenguni hulenga kwenye utimizwaji wa tumaini lililoelezwa na Uzuri Mkamilifu. Mwache Yeye Mwenyewe Awaimarishe katika kila hatua.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu